**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

***Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja unusu ukimalizia kwa maneno yafuatayo:***

*...........................................................Baada ya hotuba yake ndipo nilielewa kuwa dhuluma dhidi ya mtoto wa kike zinapaswa kutupiliwa mbali.*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Wanafunzi kila wakati hukumbushwa __1__. Hii ni kwa sababu maisha siku hizi __2__ magumu . Kama __3__ wenye ujuzi wa mambo __4__. Maana ya methali hii kuwa ikiwa __5__ vizuri manufaa ya elimu, basi tazama jinsi wale ambao hawajasoma __6__ . Hapo __7__ utatafakari yote unayoambiwa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** watie bidii | **B.** wafanye bidii | **C.** wafe moyo | **D.** waende nguu |
| **2.** | **A.** limekuwa | **B.** imekuwa | **C.** yamekuwa | **D.** zimekuwa |
| **3.** | **A.** waliosema | **B.** waliposema | **C.** walisema | **D.** walivyosema |
| **4.** | **A.** iwapo hujui chozi tazama aliaye | | **B.** asiyejua faida ya mwangaza aingie gizani | |
| | **C.** ukitaka kuvua vua na wavuvi | | **D.** zunguo la utukutu ni ufito | |
| **5.** | **A.** haujui | **B.** huijui | **C.** huyajui | **D.** huzijui |
| **6.** | **A.** wanavyokula mumbi | | **B.** wanavyokula mwande | |
| | **C.** wanavyotia fora | | **D.** wanavyotia mrija | |
| **7.** | **A.** ndimo | **B.** ndipo | **C.** ndiko | **D.** ndio |

Mtu __8__ akikosa elimu huambulia kazi za kujungujiko tu __9__ zile zenye mapato mazuri huhitaji ujuzi __10__ kupitia elimu. __11__ wa vijana ambao huidharau elimu __12__ na matatizo ya kila aina. Shida mojawapo __13__ ni kushindwa kujikimu yaani __14__ . Kwa ufupi elimu __15__ kutiliwa maanani na wote.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | **A.** wowote | **B.** yoyote | **C.** yote | **D.** yeyote |
| **9.** | **A.** almradi | **B.** ilhali | **C.** mathalani | **D.** maadamu |
| **10.** | **A.** ipatikanayo | **B.** zipatikanazo | **C.** upatikanao | **D.** upatikanayo |
| **11.** | **A.** Mkabala | **B.** Mustakabali | **C.** Aushi | **D.** Maisha |
| **12.** | A. hujazwa | B. huzalisha | C. hutingwa | D. hulikimbiziwa |
| **13.** | A. inayowakabili | B. yanayowakabili | C. linalowakabili | D. unaowakabili |

**14.** A. kuona mahitaji muhimu ya maisha
B. Kujipa mahitaji muhimu ya maisha
C. Kujipa starehe muhimu ya maisha
D. Kukwepa athari mbayanza maisha

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **15.** | A. inafaa | B. Linafaa | C. kinafaa | D. unafaa |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** Ni sentensi gani yenye kielezi cha wakati?

A. Alienda wapi baada ya kutoka huko alikokuwa ?

B. Alicheza kwa tahadhari asijiumize tena

C. Mhalifu alifungwa gerezani peke yake ingawa alitaka kutuhusisha

D. Atakapotutembelea mwakani tutamchagulia ng'ombe mnono

**17.** Bainisha matumizi ya kiambishi -ka- katika sentensi ifuatayo:

*Mwenesi ameenda shambani akachimbe makoongo*

A. Kuonyesha kufutana kwa vitendo

B. Kuonyesha kuendelea kwa kitendo

C. Kuonyesha kusudi la kitendo

D. Kuonyesha kukamilika kwa kitendo

**18.** Kutokana na kitenzi 'Vumilia', tunapata kivumishi kipi?

A. Mvumilivu

B. Kuvumilia

C. Uvumilivu

D. Mvumo

**19.** Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo;

A. Dalali alikuwa na bidhaa zifuatazo, kabati, meza, viti na rafu

B. Rita? Hujamaliza kazi hiyo nyepesi hivyo!

C. Wanafunzi wake _________ wale waliopata alama za juu zaidi _________ wametuzwa leo

D. Mkulima alipanda nafaka yaani* (wimbi na mtama)

**20.** Onyesha usemi halisi wa sentensi ifuatayo:- Mama alimwambia binti yake kuwa wangeenda shambani siku ambayo ingefuata.

A. "Mnaenda shambani kesho," mama alimwambia binti yake.

B. "Kesho nitaenda shambani," mama alimwambia binti yake.

C. "Utaenda shambani kesho," mama alimwambia binti yake.

D. "Mtaenda shambani kesho," mama alimwambia binti yake.

**21.** Tegua kitendawili kifuatacho:-

*Huku mwamba kule mwamba.*

A. Giza

B. Kaburi

C. Jiwe

D. Kioo

**22.** Chagua orodha yenye nomino za ngeli moja

A. Wembe, umbo, wayo.

B. Asali, miwani, mirathi.

C. Ulevi, wazo, mabele.

D. Shati, barua, shule.

**23.** Sentensi,
'Yaya alimfanya mtoto alale kitandani' ina maana ya
A. Mtoto alilazwa kitandani na yaya.
B. Yaya alimlalisha mtoto kitandani.
C. Yaya na mtoto walilala kitandani.
D. Mtoto alilalishwa kitandani na yaya.

**24.** Chagua sentensi ambayo ina kiambishi 'ni' cha amri
A. Nendeni mkalale sasa muda umeyoyoma
B. Mtazuru mlima Kenya lini?
C. Alinisaidia kuvuka mto huo mpana
D. Wakulima wanalima shambani.

**25.** Kanusha:
*Mtoto alipoanguka aliumia.*
A. Mtoto alipoanguka hakuumia
B. Mtoto hajaanguka wala hakuumia.
C. Mtoto asipoanguka hataumia
D. Mtoto hakuanguka na kuumia

**26.** Ni jibu lipi lenye maelezo sahihi?
A. Katikiro ni mhudumu wa ofisi anayepeleka ujumbe.
B. Sogora hutunga na kuimba nyimbo ngomeni
C. Mgema ni mraibu wa pombe nyimbo ngomeni.
D. Mjumu ni mtu anayetengeneza vitu kwa chuma.

**27.** Unganisha sentensi zifuatazo kwa usahihi.
a) Mama alienda kazini
b) Mama alikuwa mgonjwa
A. Mama alikuwa mgonjwa akaenda kazini
B. Minghairi ya mama kuenda kazini mama alikuwa mgonjwa.
C. Mama alienda kazini ingawa alikuwa mgonjwa.
D. Fauka ya kwenda kazini mama alikuwa mgonjwa.

**28.** Shairi lenye mishororo mitatu katika kila ubeti huitwaje?
A. Tathlitha
B. Thuluthi
C. Tarbia
D. Takhmisa

**29.** Chagua sentensi yenye kivumishi cha pekee?
A. Wageni wengi walitoa michango yao.
B. Wazee wale walitoa michango yao
C. Wazee wenu walitoa michango mizuri
D. Wazee wengine walitoa michango mikubwa.

**30.** Chagua jozi ambayo hailingani?
A. Simba - shibli
B. Nzige - kimatu
C. Sungura - kihongwe
D. Papa - kinegwe

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Afya au siha ni hali ya kutokuwa na maradhi. Hii ndiyo hali ambayo humwezesha mtu kuhifadhi nguvu zake za mwili na kufanikisha utendakazi katika nyanja tofauti tofauti. Mtu mwenye afya bora huweza kutekeleza mengi bila udhia. Kwa mfano, yeye huweza kujirausha na kujishughulisha hadi jioni bila kuhisi uchovu mwingi. Hata hivyo hali hii kuwa haipatikani kwa watilifu. Mwatilifu huweza kupitia changamoto nyingi hususan yule asiyejikubali.

Japo wazazi wa Tilafu waliomba Mungu wajaliwe mwana, hawakujua kuwa mwana huyo angekuwa na hitilafu za viungo vya mwili. Tilafu alikuwa miongoni mwa watoto waliozaliwa na ulemavu. Alikuwa kama watoto wengine na wakati wake wa kuenda shuleni ukafika. Japo wazazi wa Tilafu walimpeleka shuleni, hawakuwa na matumaini naye. Waliona kana kwamba walikuwa wakitumbukiza pesa zao katika jaa la takataka. Usisahau Tilafu alikopolewa akiwa na ulemavu wa kutamausha. Hata hivyo, wazazi wake walimpa mahitaji yote na kudhihirisha upendo kwake. Hii ilikuwa kinyume na mwanzoni ambapo walitaka kumsetiri ili asionekane na watu wengine waliojifungua watoto timamu kama walivyodhania wazazi wa Tilafu. Lakini baada ya kupata nasaha kutoka kwa Bi. Shauri walibadili nia na kudhihirisha mapenzi ya dhati kwa mwana wao.

Kutokana na ushauri wa Bi. Shauri, Tilafu alianza safari ya masomo akiwa na umri mrefu. Alitingwa na changamoto sufufu; kwanza angeandikaje ilhali hakuwa na mikono isipokuwa kitu kama mkono, hakuwa na miguu isipokuwa kitu kama miguu. Hata hivyo, maji ukiyavulia nguo sharti uyaoge. Alijitoa ima faima kugugumia masomo. Alijifunza kuandika akitumia kitu kama mikono alichoumbiwa na maulana. **Kumbe mungu hawezi kumnyima binadamu vyote.**

Baadhi ya wanafunzi walioumbiwa viungo vyote vya mwili walimpenda huku wengine walimponza kwa tadi na kiburi. Wengine walimwona kama kaumbwa hivyo kwa hiari yake, wengine wakashangaa atakapokuwa mkubwa atapata wapi mwandani wa ndoa, wengine walimwita hadharani kiwete au kilema huku wengine wakimnyakua na kumtaka awafuate mbio awakamate. Usisahau kuna wengi walimwumbea wasitake **kunasibishwa** naye katu.

Tilafu hata hivyo alikuwa na moyo usio na kinyongo na yeyote. Hangelipa mabaya kwa mabaya. Ajabu ni kuwa hata maadui wake waliotaka msaada wake aliwasaidia. Vilevile licha ya maumbile yake alikuwa na mwandiko mzuri kuliko mamia ya wanafunzi wenzake. Alichora picha zikazidi waliojinadi kuwa magalacha wa kuchora. Aliwachora walimu, wazazi, mahasidi na hata marafiki. Aliwashangaza wengi hata akaanza kujizumbulia riziki japo kidogo lakini kama wasemavyo wahenga, ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.

Wazazi wa Tilafu walilimatia kujuta kwa nini walimpatia kumpeleka mwanao shuleni kwa kuhofia fedheha. Kumbe ni ukweli mficha uchi hazai. Walimu wa lugha nao walianza kupendezwa na makala mengi aliyoandika yakiwa na ubunifu mkubwa na utajiri wa lugha. Mengine yalichapwa taipu na kusomwa hadharani kama ruwaza kwa wengine. Hata kiuno waliomba kupigiwa rudufu ili kila mmoja ajipatie nakala yake.

Ukweli ni kuwa Tilafu alipenda soka. Shida yake kubwa ni kuwa hakuwa na uwezo mkubwa wa kuicheza . Badala yake alikuwa shabiki sugu. Siku moja wakati wa wikendi alihiari kujikokota hadi katika uga wa michezo kushuhudia mechi ya soka. Mechi ilipokamilika washindi walishangilia kwa vifijo na nderemo na kusherehekea kwa machachari yote. Nao tandabelua hali ikawa kivangaito. Tilafu alikuwa katika harakati zake za kuguchua akirudi nyumbani.

Yarabi stara! Kundi moja la vijana lilimwinua juu juu na kumtupa pembeni mwa barabara kwa kudai kuwa anapotezea wakati na kuwazuilia njiani. Walimwacha akigaragara kwa machungu yasiyo na kifani bila kumjali. Iligharimu mkono wa wasamaria wema kumwokoa na kumkimbiza hospitalini. Akiwa hospitalini alitakiwa kumweleza mwanahabari mmoja kuhusu kilichojiri. Katika kueleza kwa ufasaha ndipo mwanahabari yule mkongwe na mwenye tajriba kubwa alipomaizi kuwa sauti ya Tilafu ilikuwa ya kipekee mno. Ilikuwa baadhi ya sauti zilizosakwa na vyombo vya habari vilivyobobea katika utangazaji. Mwana habari huyu alianza kumtafutia mbinu za kukitononosha kipaji chake siku za halafu. Kumbe ni ukweli kuwa kile unachodharau leo chaweza kuwa mwokozi wako kesho?

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, afya:
A. Huimarisha matokeo ya utendakazi
B. Humwondolea mtu matatizo mwilini
C. Humpunguzia mtu mazoea ya uchovu
D. Hukuza maendeleo katika maeneo mbalimbali

**32.** Wazazi wa Tilafu waliona kana kwamba walikuwa wakipoteza pesa zao kwa kuwa
A. hawakuona umuhimu wa masomo
B. hawakuthamini Tilafu asilani kwa kuwa alikuwa mwanaharamu.
C. hawakuwa na matumaini ya kufanikiwa kwa mwana wao.
D. Hawakuona manufaa yoyote ya kumwelimisha mtoto wao.

**33.** Kulingana na kifungu ulichosoma **si kweli** kusema kwamba
A. Bi. Shauri ndiye aliyempeleka Tilafu shuleni.
B. wazazi wa Tilafu waliweza kuonyesha upendo usio na kifani kwake
C. kulimtia kwa Tilafu kuingia katika shule kakukuathiri matokeo yake.
D. Tilafu alijizatiti kukiuka mipaka na changa moto za ulemavu wake.

**34.** Ni nini maana ya **'Kunasibishwa'** kulingana na kifungu?
A. Kusumbuliwa
B. Kuhusishwa
C. Kupatanishwa
D. Kuonekana

**35.** Sifa za Tilafu zinazojitokeza katika kifungu hiki ni
A. mwenye bidii, anayejihurumia kwa hali yake
B. mkakamavu, asiyeweka kisasi
C. mwadilifu anayetafuta kutambuliwa
D. mwenye kisasi, asiyelemewa na lolote.

**36.** Ni methali gani inayoafiki ujumbe ulio katika kauli hii?
*Kumbe Mungu hawezi kumnyima binadamu vyote.*
A. Mungu akiziba hapa huzibua pale
B. Mungu hamfichi mnafiki
C. Mvivu huguguna vifuvu
D. Mungu akikupa kilema hukupa na mwendo wake

**37.** Haki za Tilafu ambazo alikuwa amenyimwa hapo mwanzoni ni:-
A. Uhai, elimu
B. Michezo, lishe bora
C. Mapenzi , elimu
D. Elimu, ushirikiano

**38.** Kulingana na kifungu, hali ilikuwa vipi siku ya mechi?
A. Washindi walishangilia kwa shangwe na hoihoi
B. Washindi walizua vurugu kushangilia ushindi wa siku hiyo
C. Watilifu walitumwa uwanjani ili kupinga dhuluma za jamii juu yao
D. Vifijo na hoihoi vilitegemea upande wa mashiki na mashabiki.

**39.** Ni ukweli kuwa mtangazaji aliyekitambua kipawa cha Tilafu,
A. alikuwa kati ya wale waliomwokoa kutokana na hatari ya kukanyagwa
B. alikuwa na nia ya kuangazia vipawa vyake asilia
C. alimwajiri kazi katika kituo chake cha utangazaji
D. alikuwa na nia ya kuangazia masaibu aliyokumbana nayo siku ya mechi

**40.** Siku za halafu ni
A. siku za shida
B. siku za mahangaiko
C. siku za usoni
D. siku za kisogoni

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpka 50***

Ilikuwa siku ya ijumaa. Kutokana na matokeo yangu bora niliweza kuombwa kwa taadhima niwaongeleshe vijana wenzangu. **Vijana ni hewa ya kupumulia katika taifa letu**. Jambo lingine lilikuwa, mimi kuwashauri vijana wenzangu wangechangamkia kwa kuwa wangeniona mimi kama mwenzao yaani mshauri-rika. Baada ya hali kutulia nilianza hotuba yangu.

"Vijana wenzangu, leo nimejawa na furaha riboribo kwa kupata fursa hii, murwa kuweza kushiriki katika kongamano hili la kipekee. Hii ni nafasi nzuri ya kujadili maswala yanayoathiri bila kuhisi kama tunaingiliwa na yeyote. Matumaini yangu ni kuwa kukabiliana na changamoto zinazotukabili katika maisha yetu.Ninaamini kuwa nia zikiwa moja kilicho mbali huja karibu.

Ukweli ni kuwa kwa muda mrefu, tumejipata tukivutana na hata kulaumiana na wazee. Hii ni kwa sababu wao wanaona kuwa kila tufanyalo linachangiwa na upotovu. Hayo basi si kweli. Au mwaonaje vijana wenzangu? Siku zao, walisadiki kuwa kila jambo lilisababishwa na miungu. Mvua ilipoadimika, wangetoa kafara. Yangezuka maradhi kama vile **waba** na kuleta maafa , wangelilia miungu ili kupata suluhu. Hiyo ndiyo iliyokuwa mbinu yao ya kukabiliana na matatizo wakati wao.

Sote tunaelewa kuwa dunia yao ni tofauti na yetu. Sisi kizazi cha leo tunaongozwa na sayansi na teknolojia. Mvua ikiadimika tunapanda miti ili isaidie kuvuta mvua.

Tuna busara ya kuzuia maradhi kabla ya kuzuka. Aidha historia inatusaidia kujifunza kutokana na makosa waliyoyafanya enzi hizo. Japo wanasoma eti nyuma kulikuwa kweupe na mbele kweusi hatukukubaliana na haya. Cha muhimu hapa ni sote tuelewe kuwa maisha yetu yajayo yako mikono mwetu.Ulimwengu unatuendea utakavyo wenyewe. Kweli mambo hubadilika.

Hata hivyo vijana wenzangu tusije tukajihadaa. Tusiwe mwamba ngozi ambaye huvuta kwake. Kuna uwezekano wasemayo wazee wetu yana chembechembe za ukweli. Ingawa tunatawaliwa na usasa, ni dhahiri kuwa maangamizi yanayotuandama kila uchao. Iwapo hatutachukua tahadhari huenda baadhi ya nyendo zetu zikatutumbukiza katika shimo lisilo na kina. Daima laiti ningalijua.

Sina uhakika wa haya ila nilisikia kuwa katika ujana wao wazee wetu walitangamana tu kwenye vikao vya kujadili masuala muhimu au kule walikoabudu na kufanya matambiko. Hata walipoenda densini walitangamana kwa uadilifu. Kwa hakika walijistahi ipasavyo. Kijana alipomwona mzee, alimwambia kwa staha na kumfaa awezavyo. Yao haikuwa dunia ya mnyonge msonge. Umoja wao ulikuwa nguvu yao. Wana walitawaliwa na heshima mkononi na shikamoo mdomoni. Na je, kizazi chetu je? Jibu lake unalojua fika.

Jinsi nilivyoanza kwa kusema, yafaa tujiase. Faradhi tujijue. Njia ya kwanza ni kujiheshimu. Tusikubali kupotoshwa na filamu na nyimbo za kizungu tunaotazama runingani na mitandaoni. Nia na madhumuni ya waigizaji wale ni kujichumia tu. Na sisi tunaiga kama kasuku lugha yao na vitiba vyao vya kinyama. Hebu tazama kule vitiba vyao vya kinyama. Hebu tazama kule tunakokutana mara nyingi. Bila shaka ni kwenye disko, vilabuni ambako tunabugia dawa za kulevya kiasi cha kujisahau. Matokeo yake ni mimba za mapema na maradhi ya zinaa. Kuna wale hata wametuacha mikono kwa starehe za muda hata wametuacha mikono kwa starehe za muda mfupi. Tuulizane hapa waziwazi, ni nani akakiokoa kizazi chetu? Daima tukumbuke kuwa anasa hunasa kuliko uboho.

Kesho yetu inatutegemea sisi. Maisha ya kesho hujengwa na leo. Lazima tujiulize tungependa kuwa vipi hapo baadaye. Tusiwe wetu wa kubagua kazi. Tuiname cha mvunguni huku tukielewa kuwa kazi mbi si mchezo mwema. Tusingoje kubebewa na wazee wetu. Ni dhima yetu kuwachukua katika miaka yao ya ukongweni. Naam, tuwe kielezo chema kwa wale walio nyuma yetu. Asanteni vijana wenzangu. Mola awabariki nyote"

Baaada ya hotuba yangu, niliona vijana wote wamezama mawazoni wakitafakari yote niliyozungumzia.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza,ushauri marika unafaa zaidi kwani:-

A. Anayeshauriwa hujitambulisha zaidi na washauri
B. Washauri hupendekezwa na wataalam
C. Anayeshauriwa anaelewa zaidi matatizo yake
D. Washauri huwafurahisha wanaoshauriwa

**42.** Hii ni tamathali gani ya lugha inayojitokeza katika kauli hii?
*Vijana ni hewa ya kupumulia katika taifa letu.*

A. Tashbihi
B. Chuku
C. Istiara
D. Tashhisi

**43.** Kulingana na kifungu ni maelezo gani sahihi?

A. Mkutano ulihudhuriwa na wazee kwa vijana
B. Vijana walifurahi kuwa waliweza kukabiliana na changamoto
C. Mwandishi analalamikia hali ya kuingiliwa kwa masuala yao
D. Kikao kiliangazia mambo yanayowahusu vijana maishani

**44.** Badala ya **'waba'** mwandishi angesema

A. Pumu
B. Kipindupindu
C. Kishauri
D. Mba

**45.** Kulingana na aya ya tatu,

A. imani ya mtu huweza kuathiriwa na maarifa aliyo nayo.
B. matendo mengi ya vijana huchangiwa na upotovu.
C. wazee wanalaumu vijana kwa mikasa inayotokea wakati huu.
D. vijana wanaamini kuwa yaliyofanywa na wazee ni upuuzi.

**46.** Kulingana na aya ya nne, vijana wanaona fahari kwa kuwa,

A. wanayaelewa zaidi matukio ya kimaumbile
B. maisha yao yalikuwa afadhali yakilinganishwa na ya wazee
C. wana uwezo wa kuleta na kupunguza mvua watakapo
D. hawakabiliani na vizuizi vyovyote katika maisha yao

**47.** Hatibu ni mwenye hekima kwa kuwa

A. anatumia teknolojia kutabiri hali ya hewa
B. ana kipawa cha kuchunguza pande mbili za maisha yao bila mapendeleo
C. anaamini kwamba yote yasemwayo na wazee hazina msingi wowote
D. anatambua kuwa lawama za wazee hazina msingi wowote

**48.** __Jibu lake unalijua fika__. Hii inaonyesha

A. vijana wa leo ni bora kuliko wazee wa kale
B. vijana wa leo hawatawaliwi na maadili
C. vijana wa leo wanafaa kuadhibiwa vikali kwa utovu wa nidhamu
D. vijana wa leo wanafaa kuwa jela wote

**49.** Matokeo ya kwenda vilabuni na katika disko ni

A. kupata mimba za mapema na kupata magonjwa ya zinaa
B. kunywa pombe na kuelewa hali ya maisha
C. heshima ya vijana katika jamii kuongezeka
D. kuongezeka kwa watoto wengi wanaozurura mitaani

**50.** Msimamo wa msemaji ni kuwa

A. maisha yao ya baadaye yanategemea malezi ya wazee wao
B. maisha ya siku zijazo yataathiriwa na shughuli za wenzao
C. jinsi watakavyokuwa baadaye inategemea watakavyofanya sasa
D. kuishi vyema baadaye hujengwa na burudani za sasa.

Compiled & Distributed by Schools Net Kenya P.O. BOX 15509-00503, Nairobi
Tel 0734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com